**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA EWURA, BW. FELIX NGAMLAGOSI KWENYE UZINDUZI WA RIPOTI YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA MAFUTA KWA MWAKA 2016**

**UKUMBI WA LAPF DODOMA, TAREHE 19 MEI 2017**

**Mhe. Dr. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini;**

**Mhe. Dotto M. Biteko, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;**

**Wahe. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;**

**Inj. Innocent Luoga, Kaimu Kamishna wa Nishati na Petroli;**

**Prof. Eng. Jamidu Katima, Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA;**

**Wenyeviti wa Bodi Mliohudhuria;**

**Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA;**

**Wakurugenzi wa Wizara ya Nishati na Madini;**

**Wadau Mbalimbali wa Sekta Ndogo ya Mafuta;**

**Wageni Waalikwa;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana.**

**Ndugu Mgeni Rasmi**

Napenda kutumia fursa hii, kuwakaribisha wote katika mkutano huu ambao lengo lake kubwa ni kuzindua Ripoti ya Utendaji katika sekta ndogo ya Mafuta ya petroli kwa mwaka 2016. Ripoti itakayozinduliwa leo inatoa maelezo ya kina kuhusiana na biashara ya mafuta hapa nchini kwa mwaka 2016. Pia, ripoti imesheheni maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa shughuli na biashara ya mafuta nchini, ikiwemo takwimu na taarifa muhimu zinazohusiana na masuala ya mafuta ya petrol nchini kwa mwaka 2016.

**Ndugu Mgeni Rasmi,** huu ni mkutano wa kazi. Kwenye ratiba ya kazi za leo, pamoja na mambo mengine, **kwanza** utazindua Ripoti ya Utendaji katika Sekta Ndogo ya Mafuta ya Petroli kwa mwaka 2016. **Pili,** utatunuku vyeti na tuzo kwa baadhi ya watoa huduma, ambao utendaji wao katika tasnia ya biashara ya mafuta nchini katika mwaka 2016 ulionekana kuwa mzuri zaidi. Ripoti ambayo utaizindua hivi punde, ipo katika mtiririko ufuatao:

1. Sheria, kanuni na taratibu zinazotumika katika usimamizi wa sekta ndogo ya Mafuta ya petroli katika mkondo wa kati na chini ambazo ndizo nyenzo kuu zinazotumika katika utendaji wa EWURA;
2. Uagizaji, upokeaji na usambazaji wa mafuta ya petroli, hususan utekelezaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS).
3. Mwenendo wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na soko la ndani;

4. Usimamizi wa ubora wa miundombinu ya kupokelea, kuhifadhi na kusambaza mafuta;
5. Usimamizi wa ubora na usalama wa bidhaa ya mafuta ya petroli;
6. Utoaji wa leseni kwa ajili ya biashara ya mafuta ya petroli nchini;
7. Ufuatiliaji wa mwenendo wa ushindani katika soko la mafuta nchini; na
8. Mwisho Ripoti inabainisha mafanikio, changamoto za sekta hii na njia ya kupata ufumbuzi.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Ripoti utakayoizindua leo ni ya **tatu** kutayarishwa na EWURA tangu ilipotoa ripoti ya kwanza ya mwaka 2014. Ripoti hizi hutolewa kila mwaka na zimekuwa zikiboreshwa mwaka hadi mwaka ili kukidhi mahitaji ya wadau mbalimbali. Ripoti hii imejumuisha takwimu muhimu na taarifa zingine kuhusiana na uendeshaji na hali ya biashara ya mafuta kuanzia mwezi Januari hadi Desemba mwaka 2016. Ni matumaini ya EWURA kuwa taarifa hizi zitawasaidia wadau mbalimbali katika utendaji kazi kwenye maeneo yao ikiwemo maamuzi ya Kisera na kimkakati ili kuhakikisha kuwa sekta hii muhimu inaendelea kutoa mchango wake katika uchumi wa nchi yetu. Pia, takwimu na taarifa zilizomo zinasaidia kujipima na hata kujipanga vizuri zaidi, kama nchi, ili kukamata fursa zilizopo za kuvutia wafanyabiashara wa mafuta ya petrol kutumia bandari zetu za Tanzania kama lango la usafirishaji wa mafuta kwenda nchi jirani.

**Uingizaji wa Mafuta:**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika kipindi cha kati ya mwezi Januari na Disemba mwaka 2016, nchi imeendelea kupata mafuta kwa kiasi cha

kutosha kukidhi mahitaji yake. Kiasi cha mafuta ya aina zote yaliyoagizwa kupitia bandari ya Dar es Salaam na Tanga kwa ajili ya matumizi ya ndani kwa mwaka 2016 kilikuwa ni lita **bilioni 3.30** ikilinganishwa na lita **bilioni 3.34** kwa mwaka 2015 ikiwa ni pungufu kwa **asilimia 1**. Kushuka huko kulitokana na kupungua kwa matumizi ya Mafuta mazito ya viwandani (Heavy Fuel Oil – HFO) kwa asilimia 53 kutokana na kupungua kwa matumizi ya HFO kutumika kuzalisha umeme baada ya matumizi ya gesi asilia kuongezeka. Kupungua kwa matumizi ya mafuta mazito nchini ni habari njema, kwani imepunguza gharama za uzalishaji umeme na uzalishaji viwandani. Hata hivyo, katika kipindi hicho, kiasi cha mafuta ya **petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya Ndege** kiliongezeka kwa **asilimia 5** ukilinganisha na mwaka 2015. Aidha, kiasi cha mafuta yaliyoagizwa kwenda nchi za jirani kwa mwaka 2016 kilikuwa ni lita **bilioni 2.19** ikilinganishwa na lita **bilioni 1.83** kwa mwaka 2015 sawa na ongezeko la **asilimia 20**. Kwa ujumla, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani ni asilimia 65 ya mafuta yote yaliyoingia nchini wakati asilimia 35 yalikuwa ni mafuta yaliyoenda nchi jirani *(transit product).* Ongezeko la asilimia 20 la mafuta ya transit, yametokana na nchi jirani kuwa na imani na mifumo yetu ya kudhibiti ubora na uchakachuaji wa mafuta, na kuwa na mfumo mzuri wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS). **Mheshimiwa Naibu Waziri**, na wadau wa mafuta, kama nchi tujipongeze kwa kazi hii nzuri.

**Bei za Mafuta**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** katika kipindi cha mwaka 2016 bei za mafuta ghafi (*crude)* zilikuwa zikipanda taratibu kuanzia mwezi wa Januari hadi Juni na

zilishuka kidogo mwezi Julai na baadae kuendelea kupanda kuanzia mwezi wa Agosti 2016. Wastani wa bei ya mafuta ghafi (*crude oil*) katika soko la dunia kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba 2016 ilikuwa ni dola za kimarekani **42** kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa dola za kimarekani **56** kwa pipa kwa kipindi kama hicho mwaka 2015, sawa na punguzo la **asilimia 25**. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba 2016, wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilishuka kwa wastani dola za kimarekani 456, 371 na 401 kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, ikilinganishwa na wastani wa dola za kimarekani 566, 482, 507 kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2015 kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa sawia. Hii ikiwa sawa na punguzo la asilimia 22, 27 na 26 sawia

**Ndugu Mgeni Rasmi:** katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2016 bei za mafuta katika soko la ndani zilikuwa zikipanda na kushuka kwa vipindi tofauti tofauti. Hali hii ilitokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia pamoja na gharama za usafirishaji wa mafuta hayo. Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2016, wastani wa bei za mafuta katika soko la ndani kwa lita zilishuka ikilinganishwa na wastani wa bei ya mafuta katika kipindi cha mwaka 2015. Wastani wa bei za mafuta kwenye soko la ndani kwa lita katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2016 ilikuwa kama ifuatavyo; Petroli Shilingi 1,845/lita, Dizeli Shilingi 1,673/lita na Mafuta ya Taa Shilingi 1,644/lita, wakati wastani wa bei za mafuta hayo kwa lita kwa mwaka 2015 ilikuwa Shilingi 1,975/lita kwa mafuta ya Petroli, Shilingi 1,808/lita kwa mafuta ya Dizeli na Shilingi

1,739/lita kwa Mafuta ya Taa ambazo ni sawa na punguzo la asilimia 7, 8 na 6 sawia.

## MFUMO WA ULETAJI MAFUTA (BPS)

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Bei ya mafuta katika soko la ndani hutegemea thamani ya Shilingi ikilinganishwa na dola ya Marekani. Kudhoofu au kuimarika kwa shilingi kuchangia kupanda ama kushua kwa bei za mafuta kwenye soko ndani. Katika kipindi cha mwaka 2016, sarafu yetu ilidhoofu mwanzoni mwa mwaka kuanzia Januari hadi Machi 2016, na kuanza kuimarika kidogo tena kuanzia mwezi wa Aprili 2016 na kuendelea. Hali hii ilisababisha bei za mafuta katika soko la ndani kushuka kwa kiwango kidogo. Shilingi yetu ilidhoofu kutoka kiasi cha shilingi 2,144/= kwa dola mwezi Januari 2016 hadi shilingi 2,183/= kwa dola mwezi Disemba 2016. Licha ya kudhoofu kwa Shilingi yetu, wastani wa bei ya mafuta katika soko la ndani imeendelea kupungua katika kipindi cha mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa mwaka 2015 kutokana na mfumo mzuri wa usimamizi wa sekta ya petroli hususani katika uagizaji wa mafuta, na kanuni ya ukokotoaji wa bei za mafuta nchini, mifumo ambayo ni ya wazi na ya ufanisi.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja *(Bulk Procurement System – BPS*) umeendelea kutumika kuagiza mafuta nchini katika kipindi chote cha mwaka wa 2016. Mafuta yanayoagizwa kupitia mfumo huu ni Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa. Mwezi Julai 2016, EWURA iliandaa Andiko Hoja (*Discussion paper)* ilikupata maoni ya wadau juu ya

maboresho ya mfumo wa upatikanaji wa mzabuni za BPS. Mabadiliko hayo yalikuwa kutoka kwenye mfumo ambapo mshindi wa zabuni za BPS alikuwa ni mshindi wa zabuni kwa mahitaji yote ya mafuta ya nchi kutokana na wastani wa jumla wa premium *(lowest weighted average premium)* na kupendekeza mshindi apatikane kwa kwa kila mzigo (*cargo by cargo lowest premium)*. Baada ya kupata maoni ya wadau wa mafuta ya petroli, utaratibu huu ulipitishwa na Bodi ya EWURA na kuanza kutumika rasmi kuanzia mwezi wa Novemba 2016. Mabadiliko haya yamechochea ushindani ambapo ushiriki wa kampuni za ndani unategemewa kuongezeka. Aidha, gharama za uletaji wa mafuta (premiums) zimeshuka kwa kiwango kikubwa.

Kwa ujumla, katika kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Disemba 2016 meli zilizoleta mafuta ziliendelea kuja kulingana na mpangilio ambao Wakala wa Kuratibu Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (**Petroleum Bulk Procurement Agency**) na Kampuni iliyoshinda zabuni wamekubaliana. Katika kipindi hicho, Wakala wa kuratibu uagizaji wa mafuta kwa pamoja iliitisha jumla ya zabuni kumi na tisa (19) ambapo washindi wa zabuni hizo ni Kampuni zifuatazo: **Addax Energy SA ameshinda tenda (8), Augusta Energy SA ameshinda tenda (2), Sahara Energy DMCC ameshinda tenda (3)**, **Enoc Africa ameshinda tenda (2)** na **Trafigura PTE ameshinda tenda (4)**. Katika kipindi cha mwaka 2016 wastani wa gharama za uletaji wa mafuta nchini *(premium)* ulishuka kwa mafuta yote ukilinganisha na mwaka uliopita kama ifuatavyo: Petroli toka wastani wa dola 45.03/tani hadi dola 24.74/tani (sawa na asilimia 45); dizeli toka wastani wa dola 53.29/tani hadi dola 19.87/tani (sawa na asilimia 63 ); na

Mafuta ya Taa toka dola 53.27/tani hadi dola 40.76/tani (sawa na asilimia 24).

**Maghala ya Kuhifadhi Mafuta**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2016, nchi ilikuwa na maghala ya kuhifadhia mafuta (*storage depots*) yenye ujazo wa **lita bilioni 1.2.** Kati ya ujazo huo, **lita milioni 999** sawa na asilimia 92 ya ujazo, ni maghala yaliyopo Dar es Salaam. Kwa ujumla, nchi ina maghala yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi kwa zaidi ya siku mia moja ishirini (120), kwa matumizi ya nchi. Kufuatana na takwimu za 2016 uwezo wa maghala yote uliotajwa, ungeweza kuhifadhi mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani na nchi jirani kwa siku zipatazo 80.

EWURA imeendelea kusimamia uagizaji gesi itokanayo na petroli (LPG) na kukagua miundombinu yake kama vile maghala ya kuhifadhia gesi na sehemu za kujaza na kusambaza gesi (*LPG Storage and Filling Plants*) ili kuhakikisha inakidhi viwango vya ubora na usalama kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Viwango la Taifa (TBS) ama viwango vya kimataifa. EWURA imeendelea kutoa semina na uhamasishaji kwa wadau mbalimbali nchini kwa wafanyabiashara wa gesi ili kuweza kulinda afya, usalama na mazingira ya watumiaji. Kutokana na uhamasishaji kwenye bidhaa za gesi ya kupikia, makampuni yanaendelea kujenga miundombinu sehemu mbalimbali za nchi.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika kutekeleza majukumu yake ya utoaji wa leseni katika sekta ndogo ya mafuta nchini kwa mwaka 2016, EWURA

imetoa leseni mpya 151, imehuisha leseni 87, na kutoa vibali vya ujenzi 9 kwa miundombinu ya mafuta. Katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti katika sekta ndogo ya mafuta nchini, EWURA imeendelea kusimamia kuhakikisha miundombinu ya mafuta inajengwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika. Miundombinu ya zamani inaendelea kukarabatiwa ili kufikia viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Hadi sasa, jumla ya leseni 1,352 za mafuta zimetolewa katika makundi yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| a) | Waagizaji na wauzaji wa jumla | 107 |
| b) | Vituo vya mafuta | 1204 |
| c) | Waagizaji wa jumla wa vilainishi | 19 |
| d) | Ghala za mafuta | 1 |
| e) | Uagizaji wa jumla Gesi ya kupikia | 8 |
| f) | Wasambazaji wakubwa wa Gesi ya kupikia | 2 |
| g) | Wauzaji mafuta kwenye meli | 2 |
| h) | Leseni ya PBPA | 1 |
| i) | Watumiaji wakubwa wenye maghala binafsi | 7 |
| j) | Wasafishaji mafuta machafu | 1 |

**Ukaguzi wa Ubora wa Miundombinu**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2016, EWURA imeendelea kufanya ukaguzi wa miundombinu ya mafuta ili kuhakikisha inakidhi vigezo vya ubora na usalama kwa mujibu wa viwango vya TBS. Watoa huduma waliobainika kuwa na miundombinu hafifu walipewa maelekezo ya kurekebisha, ikiwa ni pamoja na kupewa adhabu

mbalimbali kulingana na sehemu kituo kilipo kwa wamiliki wa vituo vya mafuta ambavyo havijakidhi viwango. Vituo vilivyoko vijijini, miji midogo na wilayani vilitozwa faini na kupewa miezi mitatu (3) ya kurekebisha miundombinu yake ili vifikie viwango. Pia, vituo vilivyoko Manispaa, Miji mikubwa na Mikoani vilifungwa hadi pale vitakapokuwa vimerekebisha mapungufu na kukidhi viwango. Aidha miundombinu iliyokutwa imejengwa bila ya kuwa na kibali cha ujenzi (**construction approval**) kutoka EWURA ilipewa adhabu pia kwa mujibu wa Kifungu cha 126 (1) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** wote tunatambua kuwa mafuta ya petroli yasipouzwa katika mazingira stahiki na kupitia miundombinu isiyo salama na isiyokidhi viwango, yanaweza kuleta madhara makubwa. Kumekuwepo na mapokea makubwa ya wananchi kuboresha huduma za usafiri, hususan maeneo ya vijijini na kwenye miji midogo kwa kutumia vyombo vya usafiri aina ya pikipiki. Kwa kuzingatia hili, EWURA kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya mafuta, imetengeneza kanuni mpya kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini, yaani "*The Petroleum (Village and Township Retail Outlet Operations) Rules, 2014*". Kanuni hizi zinalenga kuboresha usambazaji wa mafuta hapa nchini kwani zinatoa fursa kujengwa kwa vituo vya mafuta vijijini ambavyo ni vya harama nafuu ukilinganisha na vile vinavyojengwa katika maeneo ya miji.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika kipindi cha mwaka 2016 kumekuwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) ikilinganishwa na mwaka 2015. Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi

Desemba 2016, kiasi cha gesi kilichoagizwa kilikuwa **tani 84,964** ukilinganisha na tani **70,063** zilizoagizwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia **21**. Ongezeko hili linatokana na uelewa wa watumiaji kuhusu faida za kutumia gesi na kuongezeka kwa miundombinu ya kuhifadhia, kusambaza na kujazia gesi.

**Ubora wa Mafuta**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Ni jukumu la EWURA kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli yanayosafirishwa na kuuzwa nchini. Kuanzia tarehe 1 Septemba, 2010, Serikali kupitia EWURA ilianza kuweka vinasaba (*molecular marker*) kwenye mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayotumika nchini. Programu hii ya kuweka vinasaba kwenye mafuta imepunguza kwa kiasi kikubwa uchakachuaji (*adulteration*) wa mafuta na uuzwaji wa mafuta yaliyosamehewa kodi katika soko la ndani (*tax exempted petroleum products*) na kuzuia uuzaji wa mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi jirani kupitia hapa Tanzania (*transit petroleum products*). Utekelezaji wa programu hii unafanywa kwa kaguzi za kushtukiza na upimaji wa sampuli za mafuta maeneo yote nchini na katika maeneo ya mipakani. Mwaka 2016, EWURA ilichukua sampuli kutoka kwenye vituo 807 na kupima vinasaba. Kati ya vituo hivyo, vituo 40 sawa na asilimia 5 vilikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango kuwa na vinasaba kwa kiwango stahiki. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Jeshi la Polisi, EWURA iliendesha oparesheni mbalimbali ili kudhibiti wafanyabiashara wenye nia ya kuchakachua mafuta kwa lengo la kuikosesha Serikali mapato ya kodi kwa kuingiza kwenye soko mafuta yasiyolipiwa kodi. Ni dhahiri kuwa kwa kutumia

programu hii ya vinasaba, uchakachuaji wa mafuta umepungua na makusanyo ya mapato ya Serikali yameongezeka.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Bado kuna mazingira shawishi ambayo yanaweza kupelekea uchakachuaji wa mafuta hapa nchini kuendelea, hivyo no muhimu kuendelea kutekeleza udhibiti wa ubora wa mafuta kwa kutumia njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na uwekaji vinasaba kwenye mafuta. Mazingira hayo shababishi ni pamoja na:

(a) mafuta yanayoingizwa nchini kwa ajili ya kwenda nchi jirani yanawezwa kuingizwa la ndani kinyume cha sheria (dumping of transit);

(b) mafuta ya magendo kutoka nchi jirani yamekuwa yakiingizwa nchini hasa mikoa ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa;

(c) mafuta ya miradi maalum (Tax exempted) yaweza kuingizwa kwenye soko tofauti na ilivyokusidiwa na pia

(d) mafuta ya ndege na “*condensate”* yanayotokana na uchakataji wa gesi asilia, yanaweza kutumika kuchakachua mafuta mengine.

Katika nchi yetu bado kuna vishawishi vya wafanyabiashra wasio waaminifu na kujihusisha na ukwepaji wa kodi kutokana na tofauti kubwa fedha anazopata mtu kwa ukwepaji huo. Kwa mfano kwenye mafuta ya Dizeli jumla ya kodi zote ni Tshs. 648.40 kwa lita zinapotea endapo mafuta hayatauzwa katika njia rasmi. Ambapo, gharama za uwekaji vinasaba katika lita moja ya dizeli ili kudhibiti ukwepaji huu ni Tshs. 13.50, sawa na asilimia 2 ya hela ambayo ingepotea.

## UKAGUZI WA UBORA WA MAFUTA

**Ndugu Mgeni Rasmi:** EWURA imeendelea kufanya ukaguzi ili kubaini ubora wa mafuta yanayouzwa nchini. Katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Desemba 2016, EWURA ilichukua jumla sampuli 354 kutoka kwenye miundombinu mbalimbali ikiwemo vituo vya mafuta, maghala ya kuhifadhia mafuta na magari ya kusafirisha mafuta na kuzipeleka maabara kwa ajili ya kubaini ubora wake. Kati ya sampuli hizi, sampuli 52 sawa na asilimia 14.6 hazikukudhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa (TBS).

Wafanyabiashara ambao walikutwa na mafuta ambayo hayakukidhi viwango vya ubora walipewa maelekezo ya kuhakikisha wanazingatia sheria za nchi. Pia, hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufunga miundombinu na kutoza faini kwa wafanyabiashara ambao mafuta yao yanakutwa hayana ubora wa kutosha. Aidha, EWURA imekuwa ikiwapelekea Mamlaka ya Mapato (TRA) wafanyabiashara wanaothibitika kuwa na mafuta ambayo hayajalipiwa kodi.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika kipindi cha mwaka 2016 EWURA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) imeendelea kudhibiti na kusimamia uagizaji holela wa vilainishi vya mitambo (lubricants) kwa kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanaomba leseni ya uagizaji wa jumla (*Lubricant Wholesale business licence*) kutoka EWURA kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji wa vilainishi vya mitambo vya mwaka 2014 yaani, The Petroleum (Lubricants Operations) Rules, 2014". Aidha,

EWURA imeendelea kusimamia biashara ya gesi ya kupikia majumbani (*LPG*) ili kuhakikisha taratibu husika zinazingatiwa.

**Vipaumbele kwa mwaka 2017**

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Katika mwaka 2017, EWURA itaendelea kuweka mkazo katika mambo yafuatayo katika shughuli zake za usimamizi wa Sekta ya Biashara ya Mafuta:

(a) Kuhakikisha usalama na utunzaji wa mazingira katika biashara ya mafuta unakuwa madhubuti zaidi kwa kusimamia ubora wa miundombinu ya biashara ya mafuta inajengwa na kutunzwa kulingana na sheria na kanuni stahiki.

(b) Kuhakikisha kuwa mafuta yanaagizwa na kuuzwa nchini kwa bei inayoendana na be iza mafuta katika soko la dunia.

(c) Kuendelea kuwepo mazingira mazuri ya kuwezesha ushindani wa haki katika sekta ya mafuta na kuhakikisha wadau wote wanaendesha biashara zao katika misingi linganifu.

(d) Kusimamia ubora wa mafuta nchini pamoja na ukwepaji kodi kwa kuingiza kwenye soko mafuta yasiyolipiwa kodi (transit, tax exempted products).

(e) Kuhakikisha kuwa miongozo ya ujenzi wa vituo vya mafuta vya gharama nafuu maeneo ya vijijini inasambazwa na kueleweka kwa wadau ili kuwezesha uwekezaji kwenye maeneo ya vijijini.

(f) Kuendelea kukusanya takwimu sahihi zinazohusiana na biashara ya mafuta hapa nchini.

(g) Kusimamia upatikanaji wa mafuta yenye ubora unaokidhi viwango na kwa bei inayoakisi gharama halisi kwa wakati wote na kwa nchi nzima.

(h) Kuhakikisha bidhaa ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) na mafuta mazito ya mitambo (HFO) vinaingizwa kwenye wa Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja

**Ndugu Mgeni Rasmi:** Baadhi ya changamoto ambazo zimekuwepo ni pamoja na:

(a) Kuendelea kuwepo kwa magendo ya mafuta ya taa katika mipaka ya nchi jirani katika eneo la Ziwa Victoria na mikoa ya Kanda ya Kaskazini. EWURA imeweka mkakati wa kuongeza kaguzi za kushitukiza katika maeneo hayo na kwa kushirikiana na TRA na Jeshi la Polisi..

(b) Kukosekana kwa miundombinu ya kisasa ya kusafirisha na kusambaza mafuta kama mabomba na mabehewa. EWURA imepanga kufanya utafiti ili kuanisha maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kuboresha usafirishaji wa mafuta nchini. Vilevile Serikali imekuwa ikifanya mikakati mbali mbali ya kuboresha uwekezaji kwenye miumbombinu ya kusafarishia mafuta ikiwemo mabomba na njia ya reli.

(c) Kukosekana kwa Viwango muafaka vya Gesi ya kupikia inayotakiwa kutumika nchini pamoja na Viwango muafaka vya miundombinu ya Gesi ya kupikia. EWURA inaendelea kushirikiana na TBS na wadau wengine ili kuhakikisha nchi inakuwa na viwango vya Gesi ya kupikia (LPG Specifications) vinavyofaa katika mazingira ya nchi yetu.

(d) Utumiaji mdogo wa LPG nchini unaotokana na kuwa na uwezo mdogo wa miundombinu ya kuhifadhia LPG. EWURA itaendelea kufanya uhamasishaji wa matumizi ya LPG na pia kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji katika biashara ya LPG.

(e) Uingizaji na uuzaji wa vilainishi visivyokidhi viwango na ubora unaotakiwa. EWURA imetoa maelekezo kwa kwa waagizaji wa vilainishi kupata leseni ya EWURA na kuendelea kuchukua sampuli ili kupima ubora wa vilainishi.

**Ndugu Mgeni Rasmi:** EWURA imeendelea kuleta mafanikio kwa nchi na wadau wa mafuta kwa ujumla, baadhi ya mafanikio katika mwaka 2016 ni pamoja na:

(a) Nchi kuendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa aina zote za mafuta.

(b) Kuendelea kuwa na bei za mafuta nchini zinazoshabihiana na mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia.

(c) Kuendelea kupungua kwa matukio ya uuzaji wa mafuta yasiyokidhi viwango vya ubora unaotakiwa.

(d) Kuimarika kwa ubora wa miundombinu (vituo vya kuhifadhia na kuuzia mafuta).

*(e)* Kuendelea kuwepo kwa ushindani mzuri katika soko la mafuta jambo ambalo limeendelea kuvutia wawekezaji zaidi katika sekta.

**Ndugu Mgeni Rasmi: N**apenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau mbalimbali walio katika sekta hii, ikiwa ni pamoja na: Makampuni yote ya Mafuta (OMCs), Umoja wa wauzaji wa mafuta (TAOMAC), Wamiliki wa vituo vya Mafuta (Retailers) , Umoja wa wauza mafuta wa reja reja (TAPSOA), wauzaji wa gesi ya kupikia, wasafirishaji wa mafuta, wauzaji wa vilainishi na wengine, ambao wametoa mchango mkubwa sana kufanikisha uchambuzi na maandalizi ya ripoti hii.

Aidha, EWURA inatoa shukrani za pekee kwa Wizara ya Nishati na Madini, na Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa maelekezo na miongozo inayowezesha ufanisi katika sekta hii. Shukrani nyingine ni kwa taasisi mbalimbali ambazo EWURA inashirikiana nazo ikiwa ni pamoja na: Mamlaka ya Mapato (TRA), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Wakala ya Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Shirika la Viwango (TBS), Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wakala ya Vipimo (WMA), Wakala na Nishati Vijijini (REA) na Mamlaka ya Bandari (TPA).

Mwisho napenda kuishukuru Bodi ya EWURA, Menejimenti na wafanyakazi wote wa EWURA kwa kuipitia ripoti na kutoa mapendekezo mbalimbali ya marekebisho.

**Nashukuru kwa kunisikiliza.**